JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

# TAARIFA YA UFUATILIAJI WA USALAMA WA BIDHAA ZA CHANJO NA DAWA 2021 - 2022

KANDA YA MASHARIKI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, TMDA Kanda ya Mashariki
P. O. Box 31356, Jengo la Victoria, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam
Tel: +255-737-226328/788470301, Fax: +255-22-2450793
Website: www.tmda.go.tz, Email: info.eastzone@tfda.go.tz

## 1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) pamoja na majukumu mengine, ina jukumu la kufuatilia usalama wa bidhaa za chanjo na dawa pia. Kanda ya Mashariki imetekeleza mifumo ya ufuatiliaji wa usalama wa bidhaa hizo ambayo imewekwa na Mamlaka, mifumo hiyo inajumuisha yafuatayo;

i. Ukusanyaji wa taarifa za madhara yasiyotarajiwa yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo.
ii. Uhamasishaji wa utoaji wa taarifa za madhara yasiyotarajiwa yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo.
iii. Utoaji elimu wa njia zinazotumika katika utoaji wa taarifa za madhara yasiyotarajiwa yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo.
iv. Kutathmini taarifa za madhara yasiyotarajiwa zilizoripotiwa.
v. Kudhibiti matukio ya madhara kwa wagonjwa kwa kutoa taarifa sahihi za matumizi ya bidhaa hizo.

## 2.0 HATUA YA UTEKELEZAJI

**2.1** Uhamasishaji kwa watoa huduma za afya pamoja na wananchi juu ya utoaji wa taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za chanjo na dawa hususani chanjo ya UVIKO – 19 ulifanyika katika halmashauri zote za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga ambazo ni jumla ya halmashauri **25**.

**2.2** Elimu juu ya njia za utoaji wa taarifa za madhara yasiyotarajiwa kutokana na matumizi ya bidhaa za chanjo na dawa ilitolewa kwa watoa huduma za afya pamoja na wananchi katika halmashauri zote za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga ambazo ni jumla ya halmashauri **25**.

**2.3** Fomu **2300** za kutolea taarifa za madhara yatokanayo na bidhaa za chanjo na dawa zilisambazwa katika halmashauri za Mji Kibaha, Chalinze, Kisarawe, Lushoto, Bumbuli, Rufiji, Kibiti na Mkuranga.

**2.4** Ufuatiliaji wa karibu wa usalama wa chanjo za UVIKO-19;

**2.4.1** Jumla ya watu **17,165** walipigiwa simu kwa lengo la kufuatilia maendeleo yao baada ya kuchomwa chanjo ya UVIKO-19.

**2.4.2** Watu **2,714** waliripoti kupata maudhi madogo kama homa, maumivu sehemu iliyochomwa sindano na maumivu ya kichwa baada ya kuchoma chanjo ya UVIKO – 19 ambayo yaliisha yenyewe baada ya muda mfupi.

**2.5** Vikao vya uhamasishaji wa utekelezaji wa majukumu ya TMDA ikiwemo na ufuatiliaji wa usalama wa bidhaa za chanjo na dawa kwa viongozi na watumishi vilifanyika katika halmashauri za Bagamoyo, Kibiti na Mkuranga katika Mkoa wa Pwani, manispaa za Kinondoni, Kigamboni na Temeke katika Jiji la Dar es Salaam na halmashauri ya Pangani katika Mkoa wa Tanga.

**2.6** Jumla ya ripoti **4117** za madhara yasiyotarajiwa zilipokelewa na TMDA Kanda ya Mashariki na zimehifadhiwa kwenye Vigiflow na zinaendelea kufanyiwa tathmini.

## 3.0 UTOAJI WA TAARIFA ZA MADHARA YASIYOTARAJIWA KUTOKANA NA MATUMIZI YA BIDHAA ZA CHANJO, DAWA NA VIFAA TIBA

### 3.1 Aina ya Matukio Yanayopaswa Kuripotiwa

**3.1.1** Matukio yoyote yasiyotarajiwa yatakayotokea baada ya matumizi ya bidhaa za chanjo au dawa bila kujali ukubwa wake.

**3.1.2** Matukio yanayotarajiwa lakini yamejitokeza kwa viwango ambavyo havitarajiwi.

### 3.2 Nani Anatakiwa Kuripoti?

Mtu yeyote yule anatakiwa kuripoti ikiwemo watoa huduma za afya (daktari, mfamasia, muuguzi n,k) na wananchi wote.

### 3.3 Njia za Kuripoti

**3.3.1 Fomu za kutolea taarifa za madhara**

3.3.1.1 Fomu za rangi ya njano – zinazopaswa kujazwa na wataalamu wa afya.

3.3.1.2 Fomu za rangi ya kijani – zinazopaswa kujazwa na mgonjwa au mlezi au mtu yeyote anayemuuguza mgonjwa.

**3.3.2 Kutumia simu**

3.3.2.1 Kupiga simu bure kwenda namba 0800110084

3.3.2.2 Kutumia menyu ya *152*00# na kuchagua namba 2 (Afya) kisha chagua namba 3 (TMDA) na kisha endelea kufuata maelekezo. **Njia hii ni bure pia na inatumika kwa mitandao yote ya simu.**

3.3.2.3 Kutumia *application* ya ***"TMDA ADR reporting tool"*** inayopatikana *Google Play Store.* Njia hii ni kwa watumiaji wenye simu za Android pekee.

**3.3.3** Kutuma barua pepe kwenda TMDA

**3.3.4** Kupitia tovuti ya TMDA ambayo ni www.tmda.go.tz

**4.0 HITIMISHO**

TMDA Kanda ya Mashariki inatoa wito kwa jamii kuendelea kutoa taarifa za madhara yasiyotarajiwa yatokanayo na matumizi ya bidhaa za chanjo na dawa kwani taarifa hizo ni msingi wa kuhakikisha bidhaa zinazotumika zinakidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi.

**IMEANDALIWA NA TMDA KANDA YA MASHARIKI**

**A. A. BITEGEKO**
**MENEJA WA KANDA**